



Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 26 - 2963822
Nukushi: +255 26 - 296382
Barua pepe: sg@nbs.go.tz
Tovuti: www.nbs.go.tz

Barabara ya Jakaya Kikwete
S. L. P. 2683
Dodoma
TANZANIA



Kumb. Na. BE. 424/448/01/39

Tarehe: 14 Julai, 2022

TAARIFA KWA UMMA WATALII WALIOINGIA NCHINI, KIPINDI CHA JANUARI - MEI, 2022

Taarifa ya mwenendo wa watalii walioingia nchini ni mionganini mwa taarifa za mara kwa mara (high-frequency data) zinazotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa mujibu wa **Sheria ya Takwimu SURA 351**.

Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Januari - Mei 2022

Idadi ya watalii kutoka nje ya nchi walitembelea vivutio mbalimbali vya utalii katika kipindi cha Januari hadi Mei 2022 wameendelea **kuongezeka hadi 458,048** ikilinganishwa na watalii **317,270** walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2021, ikiwa ni sawa na **asilimia 44.4 (Jedwali Na. 1)**. Kati ya watalii 458,048 walioingia nchini, watalii **137,758** waliingia nchini kupitia Zanzibar ambao ni sawa na asilimia **30.1** ya watalii wote.

Watalii walioingia nchini mwezi Mei 2022 pekee, **waliongezeka hadi 89,271** ikilinganishwa na watalii **42,173** walioingia nchini mwezi Mei 2021, sawa na ongezeko la asilimia **117.7**. Idadi ya watalii walioongezeka mwezi Mei 2022 ilikuwa zaidi ya mara mbili ya watalii walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2021.

Tanzania ni mionganini mwa nchi zenye vivutio vingi na vizuri vya utalii, ambavyo vilikuwa havijulikani sana. Kwa sasa idadi kubwa ya watalii wanaoingia nchini ni matokeo ya kazi nzuri na iliyotukuka iliyofanywa na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Filamu ya *Tanzania the Royal Tour* iliyozinduliwa nchini kwa mara ya kwanza Jijini Arusha tarehe 25 Aprili 2022. Filamu ya *the Royal Tour* imeleta mapinduzi makubwa katika Sekta ya Utalii ambapo kwa kwa sasa Tanzania inashuhudia ongezeko kubwa la watalii. Takwimu hizi zinaonesha jinsi Filamu hii ilivyofanikiwa kuongeza idadi ya watalii wanaoitembelea Tanzania.

Jedwali Na. 1: Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Kuanzia Januari hadi Mei 2022

Mwezi	2021	2022	Ongezeko	Badiliko (%)
Januari	79,116	94,441	15,325	19.4
Februari	79,730	101,042	21,312	26.7
Machi	72,285	93,889	21,604	29.9
Aprili	43,966	79,405	35,439	80.6
Mei	42,173	89,271	47,098	111.7
Jumla	317,270	458,048	140,778	44.4

Chanzo: Idara ya Uhamiaji - Juni 2022

Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Januari hadi Mei 2022 kwa Mchanganuo wa Utifa

Idadi ya watalii walioingia nchini kutoka nchi zilizo nje ya Bara la Afrika kwa mchanganuo wa utifa katika kipindi cha Januari hadi Mei 2022 unaonesha kuwa Ufaransa iliongoza kwa idadi kubwa zaidi ya watalii 28,115, ikifuatiwa na Poland ikiwa na watalii 22,651. Nchi nyingine ni Marekani (21,661), Ujeruman (16,527), Uingereza (14,136) na India (13,641).

Idadi kubwa ya watalii walioingia nchini kutoka nje ya Bara la Afrika kwa mwezi Mei 2022 pekee, walitoka Marekani (5,606), Ufaransa (4,456), India (4,211), Uingereza (3,294) na Ujeruman (3,160).

Kwa mujibu wa Sera ya Mapitio ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, takwimu za idadi ya watalii wanaioingia nchini zinaweza kufanyiwa mapitio endapo takwimu mpya na zilizohuishwa kutoka kwenye chanzo zitapatikana.

*Kwa taarifa zaidi wasiliana na Mtakwimu Mkuu wa Serikali S.L.P 2683 Dodoma,
Simu +255 26 2963822, Nukushi +255 26 296382, Baruapepe: sg@nbs.go.tz, tovuti:
www.nbs.go.tz*



Jiandae kuhesabiwa tarehe 23 Agosti, 2022